

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MPANDA
MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOKETI
TAREHE 12/11/2021 KATIKA OFISI YA MKUU WA KITENGO CHA SHERIA**

WAJUMBE WALIOHUDHURIA

- | | |
|------------------------|---|
| 1. Marietha Mlozi | Mwenyekiti |
| 2. Hobokela Mwakagamba | Katibu |
| 3. Deodatus Kangu | Mjumbe |
| 4. Dr. Paul M. Swakala | Mjumbe |
| 5. Enelia Lutungulu. | Mjumbe |
| 6. Willy Mkanga | Mshauri wa Bodi ya Zabuni (Mwanasheria) |

SEKRETARIETI

- | | |
|---------------------|------------------|
| 1. Kiloba Ahmed | Afisa Ugavi Mkuu |
| 2. Reginald Antipas | Afisa Ugavi II |

AGENDA ZA KIKAO

1. Kufungua kikao.
2. Kupitisha Agenda za Kikao.
3. Kuwasilisha na kuthibitisha Muhtasari wa kikao kilichopita cha tarehe 20/10/2021.
4. Kupitia na kupitisha taarifa ya Timu ya Tathimini ya Zabuni ya Huduma ya Usafi Eneo la Ofisi Kuu, Ukumbi wa Manispaa, Stendi ya Mizengo Pinda na Mtaa wa Buzogwe. Huduma ya Ulinzi katika maeneo mbalimbali ya Ofisi za Manispaa ya Mpanda na Usambazaji wa Chakula na Kuni katika Shule za Sekondari Rungwa na Shule ya Sekondari Wasichana Mpanda.
5. Kupitia na Kupitisha Uhuishaji wa Mpango wa Manunuzi wa mwaka wa fedha 2021/2022
6. Kupitisha Ununuzi wa Mafuta kwa ajili ya Matumizi ya Halmashauri
7. Kupitisha manunuzi yaliyofanyika kupitia waraka unaozunguka.
8. Kufunga Kikao.

MUHT. NA.MMC.101/CTB/2021/2022/03/15/01: KUFUNGUA KIKAO

Katibu aliwajulisha Wajumbe kuwa hiki ni kikao cha kawaida na kwa mujibu wa mahudhurio ya wajumbe wa kikao akidi imetimia na kuwa kikao kinaruhusiwa kufanyika, hivyo basi Katibu alimkaribisha Mwenyekiti naye Mwenyekiti aliwasalimu wajumbe. Baada ya hapo alifungua kikao mnamo saa 8:00 Mchana.

MAPENDEKEZO YA KITENGO CHA UNUNUZI

Mhe, Mwenyekiti na Wajumbe Kitengo cha Ununuzi kinakubaliana na mapendekezo ya Kamati ya Tathimini ya kutunuku Zabuni ya Usambazaji wa Chakula kikavu, Mafuta ya Taa na Kuni katika Shule ya Sekondari Rungwa kwa Mzabuni M/S Simbila (2003) General Enterprises

MAPENDEKEZO YA BODI YA ZABUNI

Bodi ya Zabuni ilipitia taarifa ya timu ya tathimini na mapendekezo ya Kitengo cha Ununuzi. Bodi ya Zabuni inapendekeza Zabuni Na LGA.101/2021/2022/CQ/G/02 ya Usambazaji wa Chakula kikavu, Mafuta ya Taa na Kuni katika Shule ya Sekondari Rungwa atunukiwe Mzabuni M/S Simbila (2003) General Enterprises

MUHT. NA.MMC.101/CTB/2021/2022/03/19/05 KUPITIA NA KUPITISHA UHUIHAJI WA MPANGO WA MANUNUZI WA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

Mwenyekiti alimkaribisha Katibu ili aweze kuwasilisha marekebisho ya Mpango wa Manunuzi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Katibu aliwaeleza Wajumbe kuwa kutokana na kupata fedha za tozo na UVICO - 19 kutoka Serikali Kuu tunatakiwa kuhuisha mpango wa manunuzi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ili kujumuisha manunuzi yote kwenye Mpango wa manunuzi.

Azimio

Wajumbe walipitia na kupitisha marekebisho ya mpango wa manunuzi kwa Mwaka wa fedha 2021/2022 yafanyike.

MUHT. NA.MMC.101/CTB/2021/2022/03/20/06: KUPITISHA MANUNUZI YALIYOFANYIKA KUPITIA WARAKA UNAOZUNGUKA

Kwa ridhaa ya Mwenyekiti, Katibu aliwapitisha Wajumbe wa Bodi ya Zabuni katika Waraka wa Manunuzi kama ifuatavyo:-

Tarehe	Maamuzi
25/10/2021	Kupitisha taarifa ya Timu ya tathimini kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya Roli na. SM13159 vyenye thamani ya Shs.2,023,100.00
25/10/2021	Kupitisha taarifa ya Timu ya tathimini kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya Roli na. SM12244 vyenye thamani ya Shs.1,528,100.00
25/10/2021	Kupitisha taarifa ya Timu ya tathimini kwa ajili ya ununuzi wa Shajala zenye thamani ya Shs.1,050,000.00 kwa ajili ya Idara ya Elimu Msingi
25/10/2021	Kupitisha taarifa ya Timu ya tathimini kwa ajili ya ununuzi wa Kompyuta Mpakato 3 zenye thamani ya Shs.4,950,000.00. Kwa ajili ya Idara ya Elimu ya Msingi
27/10/2021	Kupitisha taarifa ya Timu ya tathimini kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vyenye thamani ya Shs.790,000.00.Kwa ajili ya Kitengo cha TEHAMA
27/10/2021	Kupitisha taarifa ya Timu ya tathimini kwa ajili ya ununuzi wa Shajala zenye thamani ya Shs.370,000.00 kwa ajili ya TASAF